

# Gazeti

www.ports.go.tz | Bendera Tatu S.L.P. 9184 Dar es Salaam | Email: ccu@ports.go.tz | Namba za Bure: 0800110032 / 0800110047

## MAKAMU WA RAIS AKAGUA UJENZI WA MELI KYELA



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Kaimu Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eng. Karim Mattaka (kushoto), akitoa maelezo kuhusu ujenzi wa meli ya abiria unaondelea katika Bandari ya Itungi. Makamu wa Rais alikuwa katika ziara yake ya kikazi katika Wilaya ya Kyela Jijini Mbeya hivi karibuni ambapo pia alitembelea Bandari ya Kiwira na kukagua shughuli za Meli mbili za mizigo.

### Na Focus Mauki

**M**akamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya ziara na kukagua kazi ya ujenzi wa meli ya abiria inayoendelea katika bandari ya Itungi, Wilayani Kyela, jijini Mbeya.

Makamu wa Rais amefanya ziara hiyo Julai 28, 2018 ambapo alionyesha kuridhishwa na hatua iliyofikiwa na Mamlaka katika usimamizujenzi wa meli hiyo ya abiria.

“Nawapongeza kwa hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa meli hii ya abiria ambayo itatatua kwa kiwango kikubwa changamoto ya usafiri katika ziwa nyasa,” amesema Makamu wa Rais.

Akiwa katika bandari hiyo Naibu Makamu wa Rais alipokelewa na Kaimu Mkuugenzi

Mkuu, Eng. Karim Mattaka ambae pia alitoa maelezo mbalimbali kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa meli hiyo.

Eng. Mattaka alimweleza Makamu wa Rais kwamba mpaka sasa kazi ya uundaji wa meli hiyo itakayofahamika kama MV Mbeya II imekamilika na kazi iliyobaki ni ya kufunga vifaa mbalimbali ndani ya meli.

“Mheshimiwa Makamu wa Rais tunafurahi kukupa taarifa kwamba kazi kubwa ya uundaji wa meli hii ya abiria imekamilika kwa asilimia 75 na uundaji wa meli hii unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi disemba 2018,”

### NDANI

BANDARI YA MTWARA YAANZA KUHUDUMIA SHEHENA YA MAFUTA

03

RAIS MAGUFULI APOKEA GAWIO LA BILIONI 254 KUTOKA TPA

06

TPA MAKAO MAJUU YAHAMIA JENGO JIPYA LA “ONE STOP CENTRE

09

UVAAJI WA VIFAA KINGA NA VITAMBULISHO NI LAZIMA KWA KILA MFANYAKAZI

15

amefafanua Eng. Mattaka.

Ameongeza kwamba kazi ya uundaji wa meli hiyo ipo katika hatua ya kufunga mitambo, kuweka vyumba, kufunga viti na umaliziaji wa huduma nyingine ndani ya meli.

Mara baada ya kukamilika meli hiyo ambayo inaundwa na kampuni ya Songoro Marine itakuwa na uwezo wa kubeba

## Makamu wa Rais akagua ujenzi wa meli Kyela



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Menejimenti ya TPA na Wafanyakazi wa Kampuni ya Songoro Marine inayounda Meli ya abiria katika ziwa Nyasa wakati wa ziara yake ya kikazi katika Bandari ya Itungi hivi karibuni.

abiria 200 na mizigo tani 350 kwa pamoja.

Mwaka 2015 Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania iliamua kuunda meli tatu mbili zikiwa ni za mizigo na moja kwa ajili ya abiria na mizigo.

Meli mbili za mizigo za MV Njombe na MV Ruvuma zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja tayari zimekamilika na zimeanza kufanya kazi katika ziwa nyasa zikipeleka mizigo katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na nchini Malawi.

Ujenzi wa meli hizo ulikamilika mwezi Julai 2017 na zilisajiliwa mwaka huohuo na Mamlaka ya Udhhibiti wa Shughuli za Vyombo vya Majini (kwa wakati huo SUMATRA kwa sasa TASAC).

Gharama za uundaji wa meli zote tatu unakadiriwa kuwa ni Shilingi Bilioni 20. Mbali na kukagua ujenzi wa meli ya abiria katika Bandari ya Itungi

“

*Nawapongeza kwa hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa meli hii ya abiria ambayo itatutua kwa kiwango kikubwa changamoto ya usafiri katika ziwa nyasa,*

”

Makamu wa Rais pia alitumia ziara yake kuitembelea bandari ya Kiwira ambapo alikagua shughuli za meli za mizigo.

Mwezi Septemba 2017, meli ya MV Njombe ilifanya safari yake ya awali (maiden vooyage) kutoka Bandari ya Kiwira kwenda Bandari za Mbamba Bay (Tanzania) na Nkata Bay (Malawi).

Meli ya MV Ruvuma nayo ilifanya safari kama hiyo mwezi Januari 2018 kwa kwenda Bandari za Mbamba Bay na Monkey Bay (Malawi). Katika safari hizo meli hizo zilibeba shehena ya saruji.

Mamlaka inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba meli hizo zinaendelea kupata mizigo kutoka kwa wateja mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kupata shehena kubwa ya clinker na saruji zinazohitajika katika maeneo mbalimbali ya Tanzania na Malawi.

# BANDARI YA MTWARA YAANZA KUHUDUMIA SHEHENA YA MAFUTA

*Bandari ya mtwara sasa kujinasua kutoka katika bandari ya msimu*



Meli ya mafuta ya MV STI Brooklyn iliyobeba shehena ya mafuta tani 10,000 ikikaribia kutia nanga katika Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kupakua shehena ya mafuta mara baada ya Bandari hiyo kuanza kutoa huduma za upakuaji wa mafuta.

Na Fassie Obadia

**B**andari ya Mtwara imeanza rasmi kuhudumia shehena ya mafuta baada ya kukaa takribani zaidi ya miaka minne bila kuhudumia shehena ya mafuta. Meli ya Mv STI BROOKLYN imewasili bandarini hapo hivi karibuni ikiwa na tani elfu 10,000 za mafuta ambazo zilishushwa katika bandari hapo kongwe.

Akizungumza mara baada ya kuifunga meli hiyo Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Ubaharia, Capt. Abdullah Mwingamno amesema kwamba Bandari ya Mtwara inauwezo wa kufunga meli yenye kina cha mita kumi ikiwa na shehena ya mafuta. Kuhusu kuingiza meli hizo amesema kwamba meli hizo kwa sasa hazina shida kuingia katika lango la Mtwara kwakuwa tayari wameshafanya majaribio ya kuingiza meli na wamefanikiwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa bandari ya Mtwara, Bw. Nelson Mlali amesema kwamba anaishukuru serikali na Mamlaka kwa ujumla kwakuwa ujio wa meli hizo za mafuta utasaidia kuitoa

Bandari ya Mtwara kwenye kuwa ni bandari ya Msimu na kuiwezesha kuhudumia shehena wakati wote. Vilevile ujio wa meli za mafuta Mtwara kutasaidia kupunguza msongamano uliopo kwenye Bandari jirani ya Dar es salaam.

Nae, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Gelasius Byakanwa amesema kwamba

“

*Vilevile ujio wa meli za mafuta Mtwara zitasaidia kupunguza msongamano uliopo kwenye bandari ya Dar es salaam.*

”

anaishukuru na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutekeleza kwa vitendo ahadi zake inazofanya kwa wananchi wake kwakuwa Rais aliahidi kwamba mafuta yataanza kushushwa katika Bandari ya Mtwara.

Kwa meli kushusha mafuta Bandari ya Mtwara itasaidia Mikoa ya kusini kuwa na bei elekezi za mafuta na unafuu utakuwepo kwa watumiaji. Mkuu wa Mkoa pia amewaomba wawekezaji kuwekeza kwa wingi katika kujenga sehemu za kuhifadhia mafuta ili kuwa na visima vya kutosha. Ametoa rai kwa TRA kukamilisha mchakato wa kusafirisha mafuta kwa kupitia bandari ya Mtwara.

# MIFUMO YA MALIPO TPA KUUNGANISHWA NA MFUMO WA PAMOJA WA SERIKALI (GePG)

Na Innocent Mhando

**T**PA imewataka mawakala wa forodha na wa meli kuwa tayari kutumia mfumo wa pamoja wa malipo kieletroniki wa Serikali "Government electronic Payment Gateway System" (GePG) unaolenga kukusanya taarifa za mapato kutoka katika mifumo ya malipo ya kieletroniki katika taasisi zote za umma ikiwemo Mfumo wa TPA "Intergrated Electronic Payment System" (IePs).

Rai hiyo imetolewa na Kaimu Meneja wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Freddy Liundi wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya kuwawezesha mawakala wa Forodha na Mawakala wa meli kufahamu namna ya kutumia mfumo mpya wa malipo ya pamoja wa serikali GePG.

Akizungumzia mabadiliko hayo Bw. Liundi amesema kuwa pamoja na maboresho ya bandari yanayoendelea kwa sasa TPA pia inaendelea kuboresha mifumo ya ICT lengo likiwa ni kuwaondolea Mawakala wa forodha usumbufu na kupata huduma bora yenye uhakika na haraka hivyo katika kutekeleza hilo mifumo ya malipo ya TPA inaunganishwa na mfumo ya serikali unaoitwa GePG.

*"Wakati TPA ikiwa katika maboresha na Ujenzi wa Gati katika mradi unaoendelea pia Serikali ipo katika maboresho mifumo yake katika kutoa huduma hivyo mifumo ya Malipo ya TPA inaunganishwa na mifumo ya Serikali Kuu katika ukusanyaji wa mapato kwahiyu tukaona upo umuhimu wa kuwaita na kuwapa mafunzo haya ili muwe tayari kutumia mfumo huu wa malipo."* Amefafanua Liundi.

Ameongeza kwamba kwa kuunganishwa kwa mfumo huu wa Serikali GePG kutakuwa na faida lukuki ikiwemo kuwaondolea mawakala wa forodha usumbufu katika malipo ya TPA na pia kupata huduma ya uhakika na haraka katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Basil Baligumya akielezea manufaa ya mfumo huo amesema kuwa umeanzishwa baada ya serikali kufanya maboresho Sheria

ya usimimizi wa fedha za umma ambapo utasaidia Serikali kupata taarifa za mapato za taasisi za umma kwa wakati na kurahisisha ufanyaji wa malipo mbalimbali.

*"Mfumo huu wa malipo wa pamoja GePG utarahisisha serikali kufanya "assessment" ya makusanyo ya mapato katika taasisi zote za serikali, kupata huduma ya malipo mahali popote ulipo."* Amesema Bw. Basil.

Amesema kuwa mfumo huo utahusisha upatikanaji wa namba za malipo "Control number" ambazo zitatambulisha aina za malipo unazofanya na kukuwezesha kulipa katika njia zote za malipo simu, simbank, internet banking, na mara ukishafanya malipo mifumo ya serikali inakuwa imeshapata taarifa pia na taasisi husika.

"Hivyo malipo ya TPA badala ya kutumika namba zilizozeleka "Payment Reference Number" (PRN) kwa sasa malipo yote yatakuwa yakifanyika kupitia namba maalum za Kumbukumbu "Control Number" ambapo serikali itakuwa inatoa risiti za kieletroniki za malipo yote mtakayokuwa mnafanya " Alisisitiza Bw. Basil Baligumya.

Akielezea utaratibu wa malipo ya TPA Kupitia simu ya mkononi alisema "kupitia mtandao wa Tigopesa au M-Pesa Ukifungua Menu ya kufanya malipo chagua Lipa Bili , Malipo ya Serikali alafu itakuomba uweke namba ya malipo "Control Number" baadaye weka Pin Namba hapo utapa risiti ambapo utatumiwa kupitia ujumbe mfupi kupitia simu yako ambayo unatakiwa uitunze maana itakusaidia katika mambo mengi na tunaitambua kama ni risiti ya kieletroniki," amefafanua zaidi Basil.

Naye katibu Mkuu wa Chama cha mawakala wa Forodha Tanzania (TA-FAA), Bw. Tony Swai amewasihi wanachama wake kuendana na mabadiliko yanayoendelea katika Mifumo ya Serikali ikiwemo maboresho ya namna ya malipo katika Mfumo wa serikali (GePG) kwa kuwa unarahisisha malipo.

*"Elimu haina mwisho hivyo nawasihimu muendane na mabadiliko, elimu hii mtayoipata inamanufaa makubwa katika ufanyaji wa malipo ambayo inatazamaniwa kuondoa usumbufu wa ufanyaji wa malipo basi elimu hii ukampe na mwenzio aliyopo ofisi kwa lengo la kupata uelewa wa namna ya kutumia mfumo huu na kuendana na mabadiliko hayo ambayo yana nia njema,"* amesisita Bw. Swai.

Kwa Upande wake Muwawezeshaji kutoa Idara ya Tehama, Bw. Amri Ahmad akiongea na Gazeti hili amesema kwa kuunganishwa kwa mifumo ya TPA na Mfumo wa malipo wa Pamoja wa Serikali GePG kutaboresha ufanisi wa Bandari katika utoaji wa mizigo, utaongeza njia za malipo pia itakuwa rahisi kawa TPA na serikali kujua malipo yamefanya na nani na wapi, pia urahisi wa ufanyikaji wa "reconciliation" ambayo ni makubaliano ya malipo baina ya TPA na Mteja .

Nao mawakala wa forodha baada ya mafunzo hayo wamepongeza TPA kwa kuandaa elimu hiyo juu ya Maboresho ya mifumo katika malipo ya TPA kupitia mfumo mpya wa malipo wa serikali (GePG), pia kufanyiwa kazi kwa changamoto ambazo zinakwamisha utendaji kazi kwa kila siku.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Eng. Isack Aloyce Kamwelwe alipokutana na Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti katika ziara yake TPA ambapo pia alitamka kuthibitishwa katika nafasi yake Mkurugenzi Mkuu Eng. Deusdedit C.V. Kakoko

# KAKOKO ATHIBITISHWA RASMI KUWA MKURUGENZI MKUU

Na Focus Mauki

**W**aziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe Eng. Isack Kamwelwe amesema Serikali imemthibitisha rasmi Mkurugenzi Mkuu wa TPA mara baada ya kuteuliwa katika nafasi hiyo na kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

“

*Eng. Kakoko amepimwa na Bodi na Serikali na tumeona utendaji wake ni wa kurudhisha ambapo katika wakati wake mapato, nidhamu, mwelekeo wa shirika vimekuwa vikionekana, mfano ameweza kuishawishi Bodi na sasa meli tano zilizokuwa zimekufa kabisa zinafanya kazi, amebainisha Waziri Kamwelwe.*

”

Waziri Kamwelwe amesema Bodi ya Wakurugenzi ya TPA imempatia taarifa ya utendaji kazi wa Eng. Kakoko na inaonesha amekuwa akitimiza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu.

“Eng. Kakoko amepimwa na Bodi na Serikali na tumeona utendaji wake ni wa kurudhisha ambapo katika wakati wake, mapato, nidhamu, mwelekeo wa shirika vimekuwa vikionekana, mfano ameweza kuishawishi Bodi na sasa meli tano zilizokuwa zimekufa kabisa zinafanya kazi,” amebainisha Waziri Kamwelwe.

Ameongeza kwamba utaratibu wa kuthibitishwa katika kazi ni jambo la kawaida kabisa kwani nafasi zote za utumishi wa umma zinahitaji kufanyiwa

uthibitisho mara baada ya muhusika kufanya kazi kwa kipindi fulani “probation period”.

Maeneo mengine ambayo Eng. Kakoko anatajwa kuyafanyia kazi kwa kina ni pamoja na kusimamia kwa karibu uundwaji wa meli tatu katika ziwa nyasa ambapo kampuni ya Songoro Marine tayari imekwisha unda meli mbili za mizigo na moja ya abiria ipo katika hatua za mwisho.

Waziri pia ametaja eneo jingine ambalo Eng. Kakoko amelifanyia kazi vizuri ni pamoja na kurudhisha nidhamu ya kazi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wa nchi jirani za Zambia na Malawi ambapo Mamlaka ipo katika hatua za utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa Bandari kavu ya Inyala jijini Mbeya.

# RAIS MAGUFULI APOKEA GAWIO LA BILIONI 254 KUTOKA TPA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli akipokea mfano wa hundi kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPA, Prof. Ignas Rubaratuka na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eng. Deuseddit Kakoko.

Na Focus Mauki

**R**ais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dk. John Pombe Joseph Magufuli amepokea gawio la shilingi bilioni 254 kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Rais Magufuli amepokea gawio hilo hivi karibuni katika hafla maalumu iliyoandaliwa na ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupokea gawio kutoka kwenye mashirika mbalimbali ya Umma na kufanyika jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hundi ya gawio hilo ambalo ni sehemu ya faida iliyotokana na kufanya biashara kwa muda wa mwaka mmoja ilikabidhiwa kwa Rais Magufuli na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TPA, Prof. Ignas Rubaratuka na

Mkurugenzi Mkuu, Eng. Deuseddit Kakoko.

Gawio ambalo limetolewa na TPA kwa Serikali ni faida ambayo inatarajiwa kumrudia na kumnufaisha mwananchi wa kawaida kwa kuwa itatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayosimamiwa na Serikali.

Rais Magufuli ameishukuru TPA kwa kutoa gawio lake kwa Serikali na ameipongeza kwa kuendelea kuendesha na kusimamia biashara ya bandari ambayo inaingizia Serikali mapato makubwa na kuiwezesha kutoa

huduma mbalimbali za jamii kama vile maji na barabara.

Bodi na Menejimenti ya TPA imeahidi kuwa itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na Serikali ya Awamu ya Tano, na kuendelea kuchangia katika maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mbali na kutoa Gawio kwa Serikali ili kuunga mkono jitihada za kuboresha huduma mbalimbali; TPA pia hutoa misaada mbalimbali ya kijamii kama vile kwenye afya, elimu pamoja na huduma za jamii.



Balozi wa China nchini Tanzania, Mhe. Wang Ke akimkabidhi zawadi maalumu ya urafiki Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eng. Deuseddit Kakoko

## BALOZI WA CHINA AKAGUA UJENZI WA DMGP

Na Leonard Magomba

# B

alozi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China hapa nchini Mhe. Wang Ke leo amefanya ziara katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP).

Utekelezaji wa mradi huo mkubwa katika maendeleo ya bandari unafanywa na Mkandarasi kutoka Kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) ya kutoka nchini China.

Akiwa Bandarini, Balozi Wang Ke alipokelewa na Mkurugenzi Mkuu Eng. Deuseddit Kakoko ambaye pia alipata fursa ya kufanya mazungumzo na Balozi huyo kuhusiana na maendeleo ya mradi husika.

Mwakilishi wa Kampuni ya CHEC alimweleza Balozi huyo kwamba mradi

wa uboreshaji gati namba 1-7 mpaka sasa unakwenda kwa wakati na kwamba mpaka hivi sasa mradi umefikia asilimia arobaini ya utekelezaji ikiwa ni zaidi ya lengo kwa asilimia kumi.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inatekeleza mradi mkubwa wa maboresho ya kuipanua Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kuhudumia meli kubwa na za kisasa ambapo mara baada ya kukamilika kwa mradi huo kutaifanya bandari ya Dar es Salaam kuongeza kina chake na kufikia mita 15 hivyo kuweza kuhudumia

meli zenye uwezo wa kubeba mizigo mikubwa na kwa karaka.

Pichani ni ziara ya Balozi huyo alipokuwa Bandarini ambapo alifuatana na Eng. Kakoko. Mara baada ya ziara yake hiyo Balozi Wang Ke alimkabidhi Mkurugenzi Mkuu zawadi ya picha ya wanyama wa asili kutoka China.



Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eng. Deuseddit Kakoko akimpatia maelezo Balozi wa China nchini Tanzania, Mhe. Wang Ke kuhusiana na maendeleo ya ujenzi wa mradi wa DMGP



# WAZIRI KAMWELWE AKAGUA SHUGHULI ZA BANDARI KIGOMA

Na Mwandishi Wetu

**W**aziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Eng. Isack Kamwelwe amefanya ziara katika Bandari ya Kigoma na kukagua shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na Wafanyakazi.

Ziara ya Waziri Kamwelwe ni sehemu ya kutaka kufahamu hatua mbalimbali zilizofikiwa katika miradi mbalimbali ya TPA katika bandari za hapa nchini. Mbali na kukagua na kupewa taarifa mbalimbali Waziri pia amefanya kikao na Wafanyakazi ndani ya meli ya MV Liemba.

Meli ya MV Liemba ni meli kongwe kabisa Tanzania ikiwa bado inafanya safari zake ndani ya Ziwa Tanganyika mpaka sasa inakadiriwa kuwa na zaidi ya miaka 100 tangu ilipotengenezwa.





# TPA MAKAO MAKUU YAHAMIA JENGO JIPYA LA "ONE STOP CENTRE"

Na Focus Mauki

**O**fisi nyingi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu tayari zimehamia katika jengo jipya linalofahamika kama "TPA One Stop Centre".

Jengo hilo jipya la kisasa ambalo kwa sasa ndio jengo refu kuliko yote Afrika Mashariki na Kati lenye urefu wa ghorofa 36 lipo katika mtaa wa Azikiwe mkabala na kituo cha Mamlaka ya Forodha Tanzania (TRA) na kituo kikuu cha Polisi (central) jijini Dar es Salaam.

Lengo Kuu la kujengwa kwa jengo hili ni kuwaweka pamoja wadau wote wanaotoa huduma za Bandari kwa kuwapunguzia au kuondoa kabisa urasimu wa kutoa huduma kwa wateja na wadau mbalimbali wanaotumia huduma za Bandari ya Dar es Salaam.

Kimsingi jengo hili ambalo linafahamika kama Kituo cha Huduma za Pamoja (One Stop Centre) litakuwa na ofisi za wadau wote wanaohusika na utoaji wa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam, mfano huduma za benki.

Baadhi ya wadau wanaotarajiwa kuwa na ofisi katika jengo hilo ni pamoja na Mamlaka ya Udhhibiti wa Viwango (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tume ya Mionzi (TAEC), Mawakala wa Forodha na Mawakala wa Meli Tanzania.

Wengine ni Mabenki mbalimbali, Mamlaka ya ununuzi wa mafuta ya pamoja.

Inatarajiwa kwamba mara baada ya wadau wa bandari kuwa pamoja katika jengo hili wataunganishwa na mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kurahisisha zaidi shughuli za utoaji huduma na kupunguza muda wa kuhudumia wateja na kuongeza ufanisi zaidi katika huduma za Bandari.



Katibu Mkuu wa DOWUTA Taifa Bw. Jonathan Msoma akiongea jambo katika warsha hiyo ya siku 2



Wajumbe wakimsikiliza mtoa mada



wajumbe wakiwa makini kumsikiliza mtoa mada



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Bandari ya Dar es Salaam Menejimenti na DOWUTA wakiwa katika picha ya pamoja



Meneja Msaidizi Bandari ya Dar es Salaam Bw. Elihuruma Lema (kulia) akifungua warsha hiyo ya siku mbili iliyolenga kuwawezesha wajumbe kufahamu na kutekeleza sheria za Utumishi wa Umma na Kanuni za kazi



Wajumbe wakimsikiliza Mtoa mada (hayupo pichani)



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi DOWUTA Bandari ya Dar es Salaam Bw. Mashaka Karume akichangia jambo wakati wa semina hiyo



Meneja Utumishi Bandari ya Dar es Salaam Bw. Vitus Kapinga akiongea jambo wakati wa ufunguaji wa warsha hiyo



Wajumbe wakifuatilia mada.

# SACCOS YAPATA WAWAKILISHI MKUTANO MKUU

Na Innocent Mhando

**W**ajumbe Wawakilishi wa Mkutano Mkuu wa Bandarini SACCOS wameaswa kudumisha ushirikiano kwa lengo la kuwaleta wanachama na viongozi pamoja na kuwa mabalozi wazuri wa Chama kwa wafanyakazi

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Kukopa Bandarini SACCOS Bibi. Stella Mutayabarwa wakati akifunga uchaguzi wa kupata Wawakilishi wa Mkutano Mkuu kutoka mbalimbali uliofanyika katika ukumbi wa Zimamoto na Usalama hivi karibuni.

Amesema kuwa Chama cha Ushirika hujenga uchumi, SACCOS huwaleta watu makini pamoja, hivyo kwa dhamana waliyopewa wajumbe wapya wanapaswa kudumisha ushirikiano katika Chama ili kwa pamoja, kutimiza malengo ya Chama katika kumkomboa mfanyakazi.

“Chama cha Ushirika hujenga uchumi, SACCOS huwaleta watu makini pamoja, hivyo nawasahi Wawakilishi waliopewa dhamana ya kuwawakilisha wengine, kudumisha ushirikiano katika Chama ili kufikia malengo tuliojiwekea”. Alisema Bibi. Mutayabarwa.

Alisema pamoja na kudumisha ushirikiano, pia yawapasa kuwa mabalozi wazuri na kukitangaza Chama ili shughuli zake ziweze kujulikana kwa manufaa ya Wafanyakazi.

Aidha aliwasahi Wafanyakazi kujiunga na Chama cha Akiba na Kukopa Bandarini SACCOS kwa kuwa ina manufaa makubwa ambapo kupitia mikopo yenye riba nafuu, wengi wamefaidika, hivyo wasisite kujiunga na chama kwani ni asasi ya kifedha iliyoanzishwa mahususi kuwasaidia wafanyakazi kuweka akiba na kuweza kupata mikopo kwa riba nafuu ili kujikwamua kimaisha.

Pia Bibi. Mutayabarwa amepongeza utulivu uliokuwepo tangu chaguzi hizo zilivyoanza mpaka kufika hatua hiyo ambapo wanachama wameonesha umakini na ukomavu na kuwasahi wengine kufuata mfano ili chaguzi zimalizike kwa amani.

Msimamizi wa uchaguzi huo Afisa Ushirika Manispaa ya Temeke Bi. Jennifer Katua amewasahi wawakilishi kutimiza ahadi zao na kuwawakilisha vyema wenzao pamoja na kufuata kanuni za miongozo ya Chama.

“Nawapongeza wote kwa kushinda chaguzi hii pia dhamana mliyoipata muwawakilishe vyema wengine pia mfuata kanuni na miongozi ya Chama katika kutimiza malengo mliojiwekea” Alisema Bi. Katua.

Waliochaguliwa ni pamoja na Justicia Masinde (Utumishi), Zainab Bunduki (Ofisi ya Meneja wa Bandari) Bw. Innocent Mhando (Biashara na Masoko), Makasha waliochaguliwa ni Golden Duma, Salum Pembe, Bi. Halima Msumari, Sydney Kimisha, Paulo Malima Kafubhi, Bw. Marko B. Kalumbilo, Alexander D. Kundy na Andrew M. Nkuba.

Wengine ni Bi. Zuhura S. Maganga (Fire) Bi. Fatuma Kondo (Fedha), Bi. Alodia Mwesiga (Bandari College), Bi. Ashura Msisi (Fedha) Bi. Laizer Semahimbo (Kurugenzi ya Ununuzi na Mipango), Bi. Rabia Mahfudhi (TEHAMA), Dawali Msuya, (TEHAMA) Juma Ally (Utawala) James Mkinga (TEHAMA) Bw. Wahab

Shoo (Rasilimawatu), Mtunze Sudi (Rasilimaliwatu), kwa upande wa Marine ni Bi. Zulfa Njalumbe (KOJ) Ibrahim A. Kanuwa (Harbour Master), Jacob E. Njowoka (Hydrography), Bw. Emmanuel B. Siwale (KOJ), Maulid A. Mambi (Marine) na Zumba Mboya (Harbour Master).

Bi. Neema Pazi (TIBA), kutoka Zimamoto ni Bi. Gonsalva Mlenge, Bw. Francis Chacha Kichunge na Bw. Charles Mwakijabilwa.

Chaguzi hizo zinatarajiwa kumalizika Septemba 1, 2018 siku ya Jumamosi ambapo utamalizika na Uwakilishi wa Idara ya Nafaka na Utekelezaji.

Kwa upande wake Mwakilishi idara ya Zimamoto na Usalama Bandari ya Dar es Salaam Bi. Gonsalva Mlenge, akiongea kwa niaba ya wajumbe wenzake, amesema kuwa wanashukuru Uongozi wa Bandarini Saccos kutoa nafasi ya Wafanyakazi kupata wawakilishi ambao watawakilisha katika Mkutano Mkuu wa Ushirika na wafanyakazi wenzao kuwaamini kuwaongoza katika nafasi hiyo.

Pamoja na pongezi hizo pia wameahidi kushirikiana bega kwa bega na Viongozi wote wa Chama na Wanachama wake ili kupata mawazo ya pamoja katika kuendeleza chama na kufikia malengo ambayo chama kimejiwekea.

Pia aliwasahi Wafanyakazi kuchangamkia fursa ya uwepo wa Bandarini Saccos kiwandani kwa kujiunga na Chama cha Akiba na Mikopo Bandarini SACCOS kuweka akiba na kuchukua mikopo yenye riba nafuu ambayo itawawezesha kuanzisha miradi mbalimbali na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

# SACCOS yapata wawakilishi Mkutano Mkuu



**BI. FATUMA A. KONDO**  
KURUGENZI FEDHA HQ



**BI. ALODIA MWESIGA**  
MWAKILISHI BANDARI COLLEGE



**BI. ASHURA MSISI**  
KURUGENZI YA FEDHA



**BI. HALIMA R. MSUMARI**  
MAKASHA



**BI. JUSTICIA M. MASINDE**  
UTUMISHI



**BI. LAIZER SEMAHIMBO**  
KURUGENZI YA UGAVI NA MIKATABA HQ



**BI. NEEMA PAZI**  
MWAKILISHI HOSPITALI PHC



**BI. RABIA S. MAHFUDHI**  
MWAKILISHI TEHEMA HQ



**BI. ZAYTUNI I. BUNDUKI**  
UTUMISHI



**BI. ZUHURA S. MAGANGA**  
MWAKILISHI FIRE HQ



**BI. CONSALVA MLENGE**  
MWAKILISHI FIRE



**BI. ZULFA NJALUMBE**  
MARINE - KURASINI OIL JET KOJ



**BW. ALEXANDER DOMINIQUE KUNDY**  
MAKASHA



**BW. ALOYCE L. KAKUSA**  
KURUGENZI YA FEDHA



**BW. ANDREW M. NKUBA**  
MAKASHA



**BW. CALEB J. KULWA**  
RASILIMALI WATU HQ



**BW. CHARLES MWAKIJABILWA**  
MWAKILISHI FIRE



**BW. DAWALI S. MSUYA**  
TEHAMA HQ



**BW. EMMANUEL BAIDON SIWALE**  
KOJ



**BW. FRANCIS C. KICHUNGE**  
MWAKILISHI FIRE



**BW. GOLDEN DUMA**  
MAKASHA



**BW. IBRAHIM A. KANUWA**  
MARINE ( HARBOUR MASTER)



**BW. INNOCENT MAHANDO**  
UWAKILISHI MENEJA WA BANDARI



**BW. JACOB E. NJOWOKA - MARINE**  
MARINE - HYDROGRAPHY



**BW. JAMES MKINGA**  
TEHAMA HQ



**BW. JUMA ALLY**  
UTAWALA HQ



**BW. MARKO B. KALUMBILO**  
MAKASHA



**BW. MAULID A. MAMBI**  
MARINE



**BW. PAULO M. KAFUBHI**  
MAKASHA



**BW. SALUM A. PEMBE**  
MAKASHA



**BW. SYDNEY S. KIMISHA**  
MAKASHA



**BW. ZUMBA P. MBOYA**  
MARINE HARBOUR MASTER



**BW. MTUNZE M SUDI**  
RASILIMALI WATU HQ

# Wafanyabiashara Malawi na Tanzania WAPONGEZA JUHUDI ZA TPA KUJENGA BANDARI KAVU MBEYA



Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Eng. Karim Mattaka (wa kwanza kulia) akizungumza na Wafanyabiashara hao walipotembelea eneo la ujenzi wa mradi wa Bandari kavu.

Na Focus Mauki

**W**afanyabiashara wa kutoka nchi za Malawi na Tanzania wamepongeza juhudi na jitihada zinazofanywa na Menejimenti ya TPA za kujenga Bandari Kavu Mkoani Mbeya.

Wafanyabiashara hao wametoa pongezi hizo hivi karibuni wakati walipotembelea eneo la ujenzi wa mradi huo wa Bandari Kavu mara baada ya kuhudhuria kongamano maalumu la Wafanyabiashara wa Malawi na Tanzania lililofunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan jijini Mbeya.

Bandari Kavu hiyo inayotarajiwa kuhudumia wateja wa nchi mbalimbali jirani ikiwa ni pamoja na Malawi na Zambia, itajengwa katika eneo lenye ukubwa wa

ekari 100 lililopo katika kijiji cha Makwenje Kata ya Inyala katika Wilaya ya Mbeya vijijini.

Wakiwa katika eneo la mradi Wafanyabiashara hao walipatiwa maelezo kuhusiana na nafasi ya TPA katika kuendeleza mradi huo, maelezo ambayo yalitolewa na Kaimu Naibu Mkurugenzi Mkuu, Eng. Karim Mattaka. Eng. Mattaka aliwaeleza Wafanyabiashara hao kwamba kwa sasa TPA inafanya maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu 'feasibility study' itakayobainisha mahitaji yote katika eneo la mradi.

Mpaka sasa hatua kubwa ya upatikanaji wa eneo imekwisha kamilika, hatua itakayofuata ni ya ulipaji wa fidia kwa wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo hilo na upembuzi yakinifu ili kubainisha mahitaji muhimu na miundombinu ya mradi.

Mara baada ya ujenzi wa bandari Kavu ya Inyala kukamilika wateja wa nchi jirani za Zambia na Malawi watanufaika kutokana na kwamba umbali wa kuchukua mizigo utakuwa umepungua kwa zaidi ya kilometa 1,000.



# UVAAJI WA VIFAA KINGA NA VITAMBULISHO NI LAZIMA KWA KILA MFANYAKAZI

Na Mwandishi wetu

Wafanyakazi, wateja na wote wanaoingia katika bandari za TPA wanatakiwa kuzingatia taratibu za usalama, afya na mazingira ya bandari, kwani baadhi ya watu wamekuwa wanakiuka taratibu mbalimbali wanapokuwa ndani ya bandari.

Kuna mambo mbalimbali ambayo ni kosa kwa mfanyakazi au mtumiaji mwingine wa bandari kufanya anapokuwa ndani ya bandari. Mambo hayo ni kufanya kazi au kuingia katika maeneo ya kazi ya bandari bila kitambulisho na kuingia katika maeneo ambapo kazi za kupakuwa na kupakia mizigo na kazi zingine mbalimbali zikiwa zinaendelea bila kuvaa vifaa vya kinga (PPE) kama vile reflector, helmet, overall, mask, boots.

Aidha makosa mengine ni pamoja na kuendesha gari au chombo chochote cha moto kwa mwendokasi unaozidi kilomita 20 kwa saa, kuegesha magari/vyombo vya moto katika maeneo yasiyoruhusiwa, kuendesha gari/chombo cha moto bila kuwa na leseni husika, kuingiza bandarini magari mabovu/ machakavu, kujisaidia ovyo, kuoga katika maeneo yasiyoruhusiwa na uvutaji wa sigara ndani ya bandari.

Pia ni kosa kuosha magari katika

maeneo yasiyo rasmi, kutupa taka ovyo, mfanyakazi kuingia kazini akiwa amelewa au kuingia na kilevi bandarini, kutupa takataka au mafuta baharini na mfanyakazi kuvaa earphones anapokuwa bandarini.

Mtu yeyote atakayefanya kosa lolote kati ya makosa yaliyotajwa hapo juu atakuwa amekiuka kanuni na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni na Masharti ya Utumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari au Kanuni za OSHE.

Suala la usalama bandarini ni la kila mfanyakazi na kila mtu anapaswa kuzingatia taratibu za usalama, afya na mazingira katika eneo lake la kazi bila shuruti ili kupunguza ajali na magonjwa yanayozuilika. Wawakilishi wa OSHE kutoka kila idara muendeleo kutoa elimu ya usalama, afya na mazingira katika sehemu zenu za kazi.

Viongozi wa idara ni lazima kuhakikisha wafanyakazi walio chini yenu wana vifaa kinga wakati wote na endapo kuna wafanyakazi hawana vifaa kinga Wakuu wa Idara wawasiliane na idara ya Zimamoto na Usalama kwa ajili ya kupatiwa vifaa kinga hivyo.

EWE NDUGU MFANYAKAZI WA TPA:

**Tafadhali zingatia yafuatayo:**

- Taratibu za usalama kazini

- Pata mafunzo/maelezo ya namna ya kuendesha chombo/mashine kabla ya kufanya kazi
- Vaa vifaa vya kinga kwa usahihi muda wote unapokuwa kazini (reflector, helmet, boots, mask, overall)
- Endesha gari/chombo polepole (20km/hr.)
- Usivute sigara
- Usichafue mazingira
- Usivae earphones unapokuwa bandarini
- Inapotokea dharura toa taarifa mara moja zimamoto halafu nenda kwenye eneo la kukusanyikia (emergency assembly area)

Epuka ajali, zuia moto, jikinge na magonjwa kwani ajali/ magonjwa/ majanga husababisha:

- Vifo
- Ulemavu wa kudumu/magonjwa kama kansa, tb, n.k
- Maumivu makali mwilini
- Taifa kupoteza nguvu kazi
- Gharama kubwa za matibabu
- Kupotea kwa kipato baada ya kupoteza ajira
- Mahangaiko katika familia baada ya tegemeo la familia kuumia/kufariki
- Kuharibika kwa vitendea kazi

Fanya kazi salama urudi nyumbani salama kila siku kwa kuzingatia kaulimbiu ya Usalama kwanza/ safety first.

# WOSIA WA MDOMO HAUWEZI KUFUTA AU KUBADILISHA WOSIA WA MAANDISHI

## FAHAMU KUHUSU SHERIA YA WOSIA NA URITHI

*Wosia ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yakekuonyesha nia yake jinsi gani angependa mali yake igawanywe baada ya kufa.*

### AINA ZA WOSIA

Wosia umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni;

- Wosia wa maandishi
- Wosia wa mdomo

### SIFA ZA WOSIA WA MAANDISHI

Wosia wa maandishi ni lazima uwe na vitu vifuatavyo;

- Anayetoa wosia (Muusia) awe na akili timamu na vilevile ndani ya wosia huo ni lazima utaje kuwa mtoa wosia ana akili timamu na anahusia kwa hiari yake mwenyewe;
- Vivyo hivyo wosia huo ni lazima utaje tarehe ya siku uliyoandikwa;
- Aidha wosia wa maandishi ni lazima uandikwe kwa kalamu ya wino na si kalamu ya risasi (penseli). Sababu kuu ya Wosia kuandikwa kwa kalamu ya wino ni kuwa usiweze kufutwa wala kufutika;
- Pamoja na hayo, wosia wa maandishi ni lazima ushuhudiwe na mashahidi wanaojua kusoma na kuandika angalau wawili (mmoja wa ukoo na mwingine mtu baki), kama muusia anajua kusoma na kuandika;
- Kama Muusia hajui kusoma wala kuandika, wosia huo wa maandishi utapaswa kushuhudiwa na mashahidi wasiopungua wanne (wawili wa ukoo na wawili watu baki);

**Angalizo:** Wanaotarajia kurithi haruhusiwi kushuhudia wosia huo



au kuwa sehemu ya kuandaa wosia unaotarajiwa kuandikwa.

- Muusia atatakiwa atie sahihi katika wosia huo mbele ya mashahidi wake na kama muusia hajui kusoma wala kuandika ni lazima aweke alama ya dole gumba la kulia;
- Mashahidi wa mtoa wosia wanapaswa kutia sahihi zao mbele ya Muusia na kama hawajui kusoma wala kuandika wanapaswa kuweka alama ya dole gumba la kulia kama uthibitisho wa ushuhuda wao.

**Angalizo:** Mashahidi wa Wosia huo ni lazima wawe wamechaguliwa na muusia mwenyewe.

**IFAHAMIKE KUWA:** Wosia wa maandishi unaweza kubadilishwa kwa wakati wowote na mtoa wosia kwa kuandaa wosia mwingine wa maandishi na kufuata taratibu zilizoainishwa hapo juu ambapo ndani ya wosia huo mtoa wosia atataja kubadilisha wosia wa awali.

### SIFA ZA WOSIA WA MDOMO

Wosia wa mdomo lazima uwe na vitu vifuatavyo;

- Mtoa wosia (Muusia) awe na akili timamu;
- Ni lazima ushuhudiwe na mashahidi wanne (wawili wa ukoo na wawili watu baki);

**Angalizo:** Mashahidi wa Wosia huo ni lazima wawe wamechaguliwa na muusia mwenyewe.

**IFAHAMIKE KUWA:** Kwa Wosia wa mdomo, ikitokea mashahidi wakafariki kabla ya mtoa Wosia, basi wosia hautakubalika na urithi utagawanywa kama urithi usio na wosia. Hata hivyo, Muusia kama bado ana nia ya kuusia mali zake atapaswa atoe wosia mpya.

**KIMSINGI,** Sheria inaweka wazi kwamba kuandikisha wosia sio lazima, bali ni hiari ya muusia. Aidha ikumbukwe kuwa, wosia wa mdomo hauwezi kufuta au kubadilisha wosia wa maandishi. Hata hivyo, wosia wa maandishi unaweza kufuta au kubadilisha wosia wa mdomo ikiwa waliokuwa mashahidi wa wosia wa mdomo watashiriki.

IMEANDALIWA NA:

SALMA KITWANA NA

CHRISTIAN CHIDUGA

IDARA YA HUDUMA ZA SHERIA

MAMALAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)